

Usimulizi Unavyoibua Dhamira katika Tamthiliya ya Kiswahili: Uchambuzi wa *Tendehogo*

*Elizabeth G. Mahenge*¹

Ikisiri

Makala imechambua namna usimulizi unavyoibua dhamira mbalimbali katika tamthiliya ya *Tendehogo* kwa kutumia mkabala wa kinaratolojia, unaochunguza namna usimulizi unavyofanyika katika simulizi. Nadharia ya Naratolojia ilitumika kuchambua sauti za usimulizi zinazojitokeza. Sauti hizi za usimulizi zimetuwezesha kujua mtazamo wa msimulizi kwamba anasimulia akiwa ndani ya simulizi, ikimaanisha kuwa anaunga mkono yanayosimuliwa; hili linabainika kwa kutumia nafsi ya kwanza ya usimulizi. Pia, msimulizi anasimulia akiwa nje ya simulizi, ikimaanisha kwamba haungi mkono masimulizi, hili linabainika kwa kutumia nafsi ya tatu ya usimulizi. Kitendo cha msimulizi kuwa ndani au nje ya simulizi katika Nadharia ya Naratolojia, kina uhusiano mkubwa na kile kinachosimuliwa. Akisimulia kwa nafsi ya kwanza (anaunga mkono na yuko ndani ya simulizi), akisimulia kwa nafsi ya pili (anaunga mkono, yuko ndani ya simulizi, na anamhusisha msomaji ili achukue hatua katika simulizi), akisimulia kwa nafsi ya tatu (haungi mkono, yaani amejitenga na yuko nje ya simulizi). Dhamira zimesawiriwa kupitia kauli za wahusika ambazo zinajidhihirisha kwa kutumia sauti za usimulizi zinazojibainisha kama nafsi ya kwanza, ya pili na ya tatu. Matokeo ya utafiti huu yameibua aina mbalimbali za dhamira zikiwamo mapenzi, usaliti na unafiki, kwa kutaja kwa uchache. Mapendekezo yanayotolewa na utafiti huu ni kufanya utafiti mwingine katika tamthiliya hii ili kuchunguza namna sauti za usimulizi zinavyoweza kuibua aina mbalimbali za utumwa katika *Tendehogo*.

1.0 Utangulizi

Utumwa ni mfumo wa maisha katika jamii ambapo mtu mmoja humiliki watu wengine kama mali na huwalazimisha kufanya kazi au jambo fulani bila malipo au ridhaa (BAKITA, 2015; TUKI, 2019; Henry, 2020). Miers (2000) anauelezea utumwa kama mfumo unaomiliki watu na kuwafanyia chochote unachotaka; unaweza kumuuzwa au kumnunua mtu, na unaweza kumrithi na kumtoa kama zawadi. Fasili hizi zinatupatia mambo kadhaa kuhusu utumwa kwamba ni mfumo, unalazi-

¹ Mhadhiri Mwandamizi, Idara ya Fasihi, Mawasiliano na Uchapishaji. Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania. Barua pepe: lizmahenge@udsm.ac.tz

misha kufanya jambo au kazi, na kwamba mtumwa hana sauti juu ya maisha yake. Hata hivyo, kuna baadhi ya tafiti zinazoelezea utumwa kama jambo la hiari na kwamba kipengele cha 'kulazimishwa' hakipo (van der Linden, 2017). Haifahamiki ni lini utumwa ulianza katika jamii bali umekuwapo katika jamii mbalimbali kama sehemu ya mfumo wa maisha ya watu. Tena umekuwa ukibadilika kutokana na mahitaji na mabadiliko ya kimazingira na kimuktadha.

Miers (2000), Welch (2009) na Henry (2020) wanaenda mbele zaidi kwa kubainisha aina mbalimbali za utumwa, ukiachilia mbali ule wa kijadi. Kwa mujibu wa maelezo yao, kuna utumwa wa kisasa unaojidhihirisha kupitia fikra, ajira ya watoto wadogo, ndoa za kulazimishwa na za utotoni, kukimbilia ughaibuni, utumwa wa kidini, kazi za kulazimishwa na utumwa wa madeni. Japokuwa watafiti hubainisha aina hizo kama utumwa wa 'kisasa' lakini ni aina za utumwa ambazo zimekuwapo tangu kale. Kuwapo kwa utumwa katika jamii kunawafanya wasanii kama vile watunzi wa kazi za kifasihi kulisawiri jambo hilo katika kazi zao kama ilivyojitokeza katika tamthiliya ya *Tendehogo*. Hili linathibitisha uhusiano uliopo kati ya jamii na fasihi kwa kuwa fasihi haitokani na ombwe tupu bali hutumia malighafi zilizopo katika jamii (Semzaba, 1977; Madumulla, 2000; Mulokozi, 2017).

Kuna tafiti mbalimbali katika fasihi ya Kiswahili zinazochunguza suala la utumwa kama vile Mutembei (2001), Henry (2020) na Mulokozi (2020). Mutembei (2001) alichambua dhamira ya utumwa akiangalia ni kwa namna gani watunzi wa fasihi ya Kiswahili wamelisawiri suala la utumwa kwa kipindi cha miaka hamsini akichunguza kazi tatu ambazo ni: *Uhuru wa Watumwa* (1934), *Maisha ya Tippu Tip* (1966) na *Tendehogo* (1984). Mutembei alitafiti ili kubaini uelewa wa utumwa na changamoto zake katika jamii ya Waswahili. Utafiti huo umetupatia mwangaza kuhusu uelewa wa wanajamii kuhusu suala la utumwa ambalo limekuwapo kwenye jamii hiyo kwa miongo kadhaa. Pia, utafiti wake umetuwezesha kufahamu uelewa wao kuhusu changamoto zilizotokana na utumwa huo mkongwe.

Henry (2020) alichambua riwaya ya *Uhuru wa Watumwa* akiangazia simulizi za watumwa kupitia ruwaza, motifu na maudhui. Katika utafiti huo alichunguza jamii za Kiafrika, Kimarekani na Kiulaya ili kuona ni kwa vipi simulizi za utumwa zinasimuliwa na kama kuna muumano au mwachano wowote. Utafiti wake ulibaini kwamba licha ya utofauti wa miktadha ya kiutunzi kati ya jamii hizo, kumekuwapo na matumizi ya ruwaza tofauti kutoka jamii moja hadi nyingine kutokana na tofauti za kitamaduni. Hata hivyo, simulizi hizo zina masuala yanayofanana. Kazi ya Henry imetuongezea maarifa kwa sababu imetuwezesha kufahamu kwamba, japokuwa jamii hizi tatu zinatofautiana katika muktadha na nduni, zina mambo yanayofanana. Kazi yake imetuwezesha pia kufahamu kwamba utumwa ni utanzu mahususi wa kifasihi wenye nduni anuwai za kisanaa.

Naye Mulokozi (2020) aliangazia harakati mbalimbali zilizofanywa na watu weusi duniani kwa lengo la kuungana. Mulokozi anaelezea historia ya utumwa katika bara la Afrika na ughaibuni, na jinsi jamii hizi mbili zilivyopitia uzoefu huo

wa kimaisha kwa namna mbalimbali. Anaeleza kuwa biashara ya watumwa kati ya Afrika na Asia ilishamiri kabla Waafrika hawajaanza kupelekwa utumwani Ulaya na Amerika. Anaendelea kufafanua kwamba kunako karne ya 15, Waafrika kutoka barani Afrika walianza kuuzwa kwa wingi utumwani huko Ulaya na Amerika kama nguvukazi katika mashamba, migodi na viwanda. Hata hivyo, kabla ya kipindi hicho, katika bara la Afrika kulikuwapo na aina ya utumwa wa ndani kwa ndani ambapo watu wenye uwezo, mamlaka ya kiutawala na ushawishi katika jamii waliwafanya baadhi ya watu kuwa watumwa. Mambo haya yalitokea kwa kuwa jamii nyingi za Kiafrika zilikuwa zinaishi katika hali ya utengano. Hakukuwa na umoja imara wala dola thabiti ya watu weusi duniani ambayo ingeweza kupingana au kushindana na hali hizo za kufanywa watumwa au kupelekwa utumwani.

Mulokozi (2020) anafafanua suala hili akigusia mkutano wa Berlin wa mwaka 1884/5 uliojumuisa mataifa makubwa ya Ulaya yakiongozwa na Ujerumani, ambayo yalikutana Berlin-Ujerumani kwa ajili ya kuligawa bara la Afrika kwa kadiri yalivyotamani. Baada ya mkutano huo, mataifa hayo yalipata uhalali wa umiliki na hivyo yakaingia barani Afrika kwa nguvu za kijeshi ili kuchukua “mgawo” wao. Unyonge wa watu weusi wakati huo, uliwafanya wasiweze kushindana nao. Viongozi wa kijadi walikubali kujiweka chini ya Wazungu isipokuwa katika jamii chache Wazungu walikutana na upinzani. Miongoni mwa jamii za Watanzania zilizopinga uvamizi wa Wajerumani katika Ujerumani ya Afrika Mashariki (sasa Tanzania Bara) ni watu wa Pwani (1888), Wayao (1892), Wanyamwezi (1891-1892), Wahehe (1891-1898), Wachaga (1892), na jamii za kusini mwa Tanzania ambazo zilipinga uvamizi huo kupitia Vita vya Majimaji (1905-1907). Mawazo yanayoibuliwa na Mulokozi ni muhimu kwa kuwa yanatupatia mwangaza wa kuona kwamba suala la utumwa lilikuwapo barani Afrika hata kabla watu wa bara la Asia hawajaingia Afrika.

2.0 Umuhimu wa Usimulizi katika Tamthiliya

Tamthiliya ya *Tendehogo* ni zao la jamii na tunaona uhusiano wake kwa jamii mbili zilizohusika kwenye biashara ya utumwa - jamii za Waafrika na Waarabu. Je, kwa nini ni muhimu katika utafiti huu kuchunguza tamthiliya? Ni muhimu kwa sababu ni utunzi pekee wa kifasihi unaoweza kumithilisha maisha jukwaani (Semzaba, 1977) kuhusu utumwa na biashara ya utumwa. Hii ni kutokana na uwezo wake wa kuyaweka maisha halisi jukwaani, tofauti na kumbo zingine kama vile ushairi, riwaya au hadithi fupi. Mbali na *Tendehogo* (Semzaba, 1984), zipo kazi kadhaa za fasihi ya Kiswahili ambazo zimesawiri dhamira ya utumwa kama vile *Uhuru wa Watumwa* (Mbotela, 1934), *Kasri ya Mwinyi Fuad* (Shafi, 1987), *Kwaheri Iselamagazi* (Mapalala, 1992), na *Miradi Bubu ya Wazalendo* (Ruhumbika, 1995) kwa kutaja kwa uchache. Kutokana na hoja ya umithilishaji wa maisha jukwaani *Tendehogo* ilionekana ni mujarabu kutafitiwa tofauti na kazi zingine zilizotajwa.

Edwin Semzaba ni mtunzi aliyeandika kazi nyingi za tamthiliya, zikiwamo *Mkokoteni*, *Joseph na Josephine*, *Kinyamkera*, *Tendehogo* na *Ngoswe Penzi Kitovu*

cha Uzembe. Hata hivyo, kazi zenye umaarufu ni *Tendehogo* na *Ngoswe Penzi Kitovu cha Uzembe*. Umaarufu wa kazi ya *Tendehogo* unatokana na aina ya dhamira inayoshughulikiwa na, hivyo, kusababisha kuibuka kwa mijadala ya kitaaluma. Vilevile, *Ngoswe Penzi Kitovu cha Uzembe* ni tamthiliya ambayo imekuwapo katika mfumo wa elimu ya sekondari nchini Tanzania kwa miaka mingi.

Kazi hii ya *Tendehogo* imeteuliwa kutokana na umaalumu wake kwa sababu inaendana na dhamira ya makala hii. *Tendehogo* ni tamthiliya inayoelezea jinsi biashara ya watumwa ilivyofanywa na wafanyabiashara Waarabu na wenyeji katika Afrika Mashariki mnamo karne ya 18 na 19. Tamthiliya inasimulia kuhusu uzoefu wa watumwa wa Kiafrika walivyonyanyaswa na mfanyabiashara Harun na kuwapeleka Bara Hindi ambako ni mbali na kwao. Makala hii ilichambua *Tendehogo* ili kuona ni kwa namna gani mwandishi wa tamthiliya hii anatumia 'sauti za usimulizi' ili kuibua dhamira. Lengo la kufanya hivyo ni kuonesha kuwa matumizi ya sauti za usimulizi yanaweza kutumika kama mbinu ya kuibua dhamira katika kazi za kifasihi. Kwa kuongozwa na Nadharia ya Naratolojia, makala hii imefafanua aina mbalimbali za sauti kupitia nafsi za usimulizi zinazojitokeza na maana inayoibuliwa kwa matumizi hayo.

3.0 Methodolojia

Tendehogo ni tamthiliya inayohusu utumwa mkongwe kati ya Tanganyika na Bara Arabu. Makala hii ilichambua tamthiliya ya *Tendehogo* ili kuona ni kwa namna gani mwandishi wa tamthiliya hii anazitumia 'sauti za usimulizi' ili kuibua dhamira. Sauti za usimulizi ni zile nafsi zinazotumika katika kusimulia simulizi, yaani viwakilishi vya nafsi ambavyo nia *mimi*, *wewe* na *yeye* katika umoja; na *sisi*, *nyinyi* na *wao* katika wingi. Lengo la kufanya hivyo ni kuonesha kuwa matumizi ya sauti za usimulizi yanaweza kutumika kama mbinu ya kuibua dhamira katika kazi za kifasihi. Kwa kuongozwa na Nadharia ya Naratolojia, makala hii imefafanua aina mbalimbali za sauti kupitia nafsi za usimulizi zinazojitokeza na maana inayoibuliwa kwa matumizi hayo.

3.1 Muhtasari wa Tamthiliya Teule

Tendehogo ni tamthiliya ya Kiswahili iliyoandikwa na Semzaba na kuchapishwa na Tanzania Publishing House (1984). Tamthiliya hii inaelezea jinsi biashara ya watumwa ilivyofanywa na wafanyabiashara Waarabu katika Afrika Mashariki mnamo karne ya 18 na 19. Tamthiliya inasimulia kuhusu uzoefu wa watumwa wa Kiafrika walivyonyanyaswa na mfanyabiashara Harun na kuwapeleka Bara Hindi ambako ni mbali na kwao.

3.2 Nadharia ya Naratolojia

Utafiti huu umeongozwa na Nadharia ya Naratolojia ili kufikia malengo ya utafiti. Hii ni nadharia inayofafanua namna usimulizi unavyofanywa na msimuliaji (Bordwell, 1985; Bal, 1997). Kupitia nadharia hii, tunaweza kufahamu mtazamo wa

msimulizi anayesimulia hadithi yake na hivyo kutuwezesha kufahamu ni nani anayeongea kama ni msimulizi-mhusika, msimulizi aliye nje ya usimulizi au wakala anayeachwa na msimulizi ili asimulie badala yake.

Kwa mujibu wa Genette (1980) na Bordwell (1985), nadharia hii ina misingi mikuu mitatu: hadithi, usimulizi na ploti. Msingi wa kwanza ambao ni hadithi unahusu mhusika wa hadithi au wakala anayesimulia hadithi hiyo. Huyu anaweza kuwa ni mhusika mkuu au mdogo. Pia, anaweza kuwa ni mhusika mviringo au bapa. Msingi wa pili ni usimulizi ambao huchunguza namna hadithi inavyosimuliwa (yaani kwa mtazamo wa nani hadithi inasimuliwa); je, ni kwa mtazamo wa nafsi ya kwanza, ya pili au ya tatu? Katika msingi huu wa usimulizi, kila nafsi inayotumika kusimulia ina maana yake. Msingi wa tatu ni ploti ambayo ni mpangilio au mtiririko wa simulizi unavyofanywa kama ni moja kwa moja, ikimaanisha kuwa hadithi inaanzia mwanzo na kuendelea hadi mwisho wake, au kwa mtindo wa kioo, yaani nyuma-mbele, ikimaanisha kuwa hadithi inaanzia mwisho na kurudi mwanzo (Bordwell, 1985) ambao Bal (1997) anauita fabula² kama tutakavyoona.

Uchambuzi wa makala hii umeongozwa na msingi wa pili wa Nadharia ya Naratolojia ambao unahusika na namna usimulizi unavyofanyika. Nadharia hii ina historia ndefu kuanzia kwa Vladmiri Propp katika kazi yake ya *Morfologiya skazki* ya mwaka 1928 iliyochunguza muundo wa simulizi katika hadithi (Jann, 2005). Nadharia hii iliendelea kuvutia wananadharia mbalimbali ambao waliitumia kwa mielekeo au maelezo tofauti kulingana na fani zao za kiutafiti na kiuchambuzi. Katika makala hii, nadharia hii inatumia kama inavyoelezewa na Genette (1972/1983) na Bal (1997) ambao wanachunguza usimulizi unavyofanywa na msimulizi. Bal anaenda mbali zaidi kwa kutazama kila tukio katika maisha kama 'aina' fulani ya usimulizi (Bal, 1997).

3.3 Sauti za Usimulizi katika Nadharia ya Naratolojia

Hadithi inavyosimuliwa inaweza kutumia sauti tofautitofauti ambazo tunazibaini kupitia mitazamo ya usimuliaji. Mathalani, msimulizi (mtu anayesimulia hadithi) akisimulia kwa kutumia nafsi ya kwanza, ya pili au ya tatu, kunakuwa na athari tofauti kwa hadhira (wasomaji). Msimulizi akisimulia kwa nafsi ya kwanza na ya pili, anakuwa karibu na simulizi wakati akisimulia kwa kutumia nafsi ya tatu anakuwa mbali na simulizi. Katika kitabu chao cha *Handbook of Narrative Analysis*, Herman na Vervaeck (2005) wanaelezea kuhusu maswali matatu muhimu ambayo ni *nani*, *nini* na *kwa vipi*. Katika kulijibu swali la "nani" wanaelezea aina mbili za sauti za usimulizi: usimulizi kwa ngazi ya juu na usimulizi kwa ngazi ya chini.

Sauti ya usimulizi kwa ngazi ya juu inamaanisha kuwa msimulizi anafahamu kila kitu kuhusu simulizi na hivyo anajitokeza kwa nafsi ya tatu. Hivyo, sauti ya

² Fabula ni mtiririko wa kimantiki na kimfuatano unaosimulia kuhusu tukio linalosababishwa na wahusika katika matini; ni jinsi wahusika wanavyopangilia visa vya hadithi waitoayo tangu mwanzo hadi mwisho.

usimulizi kwa ngazi ya juu inajitokeza pale msimulizi anapokuwa ni mtazamaji na siyo mtendaji, yaani msimulizi siyo mhusika katika hadithi. Hoja hii ni kama ilivyoelezewa na Mlacha (1991), Mohochi (2000) na Madumulla (2009) kuhusu msimulizi mwakote kwamba ana uwezo wa kujua kila kitu kinachoendelea hata katika fikra za mhusika.

Kwa upande mwingine, Herman na Vervaeck (2005) wanaelezea kuhusu sauti ya usimulizi kwa ngazi ya chini kuwa, ni pale msimulizi anapojitokeza kama mhusika katika hadithi kwa nafsi ya kwanza akisimulia na kuelezea uzoefu wake. Kwa mujibu wa Bal (1997) sauti hii iko kwenye darajia la kwanza, ambalo linamaanisha msimulizi ni mtendaji. Mgawanyo wa sauti za usimulizi kwa mujibu wa Herman na Vervaeck (2005) unashindwa kuitambua nafsi ya pili kama mojawapo ya sauti ya usimulizi.

Mathalani, Matt (2003) anaeleza kuwa, kuna haja ya kupitia upya mgawanyo wa sauti za usimulizi kwa kuwa nafsi ya pili ambayo hapo awali haikutambulika kama mojawapo ya sauti za usimulizi, siku hizi inatumika katika simulizi. Herman na Vervaeck (2005) hawaitambui nafsi ya pili kama “sauti ya usimulizi” kama yalivyo mawazo ya Madumulla (2009). Madumulla anakiri kuwa nafsi ya pili “haitumiki katika usimulizi” bali inatumika katika mazungumzo ya kawaida. Kwa mujibu wa tafiti za mbalimbali zilizofanyika kuhusu “nafsi ya pili” ya usimulizi, baadhi ya wachambuzi wa kifasihi wanatambua nafsi ya pili kama sauti ya usimulizi (Matt, 2003; Fludernik, 2006; Mahenge, 2019). Nafsi ya pili ya usimulizi ikitumika kusimulia hadithi inamaanisha msomaji anatakiwa atimize jukumu fulani katika kukamilisha simulizi inayotolewa. Fludernik (2006) anaendelea kueleza kuwa msimulizi akitumia sana nafsi ya pili pamoja na njeo ya wakati uliopita /li/, ndipo msomaji anapogutuka na kufahamu kuwa msimulizi hazungumzi na yeye (msomaji halisi) bali anazungumza na msomaji wa kufikirika ambaye (mwandishi na msimulizi) walimfikiria walipokuwa wanaandika na kuisimulia kazi yao. Lakini msimulizi akitumia “nafsi ya pili” pamoja na “njeo ya wakati uliopo” (yaani wakati wa sasa hivi) /na/ ndipo msomaji anajichukulia jukumu kwamba ni ‘yeye’ anayeambiwa ili atende jambo fulani (Mahenge, 2019).

4.0 Dhamira Zinazoibuliwa katika Tamthiliya ya *Tendehogo*

Katika sehemu hii, dhamira zilizoibuliwa katika tamthiliya ya *Tendehogo* zimewasilishwa na kujadiliwa. Kwa kutumia uchambuzi wa kinaratolojia wa sauti za usimulizi, makala imeweza kuibua dhamira mbalimbali ikiwamo: kutokujitambua, mapenzi, unafiki, ukombozi wa kifikra na mapinduzi.

4.1 Kutojitambua

Kutokujitambua ni aina mojawapo ya dhamira ambayo inajitokeza katika tamthiliya hii. Chonge anashindwa kujitambua yeye ni nani na thamani yake ni ipi kwa kuwa anakubali kutumiwa na Harun ili awanyanyase wenzake. Badala ya Chonge kuzinduka na kuwa upande mmoja na watumwa wenzake, yeye ndiyo kwanza

anatafuta habari nyeti ili azipeleke kwa boshi wake kwa lengo la kuwashtakia watumwa wenzake, yaani kwa Harun. Kutokujitambua kunazuia uwezo wa kufikiri alionao mtu kwa sababu eneo lake la ufahamu ‘limetekwa nyara’. Jambo hili linamfanya Chonge kukosa ufahamu kuhusu maisha yake na umuhimu wa kuwa huru, kwa kuwa haoni faida ya kubadilisha hali yake ya kimaisha na anaendelea kutarajia maisha bora huko Bara Arabu. Msimulizi kupitia mazungumzo kati ya Chonge na Maugwaju anasema hivi:

Maugwaju: Lakini si kuna mpango?

Chonge: Achana na mipango isiyo na misimamo watamuweza wapi
Harun

(Semzaba, 1984: 13).

Msimulizi anatumia nafsi ya tatu kusema mawazo yake kupitia kwa mhusika Chonge kwamba, “achana na mipango isiyo na misimamo watamuweza wapi Harun” (Semzaba, 1984: 13). Hii inamaanisha msimulizi ni mtazamaji, yuko nje ya simulizi na hakubaliani na wazo la Chonge maana ni mtu asiyejitambua.

4.2 Mapenzi

Mapenzi ni aina nyingine ya dhamira ambayo imejitokeza katika tamthiliya ya *Tendehogo* ikimhusisha Maugwaju na Chonge. Chonge anatumia maneno ya ulaghai kwa mhusika Maugwaju ili aweze kupata ngono kwa njia za hila. Mathalani, Chonge anamrubuni Maugwaju ili amsaliti mchumba wake na kumkubali yeye ambaye hampendi kwa dhata ila anataka tu kufaidi huduma ya kingono. Maugwaju anakataa ulaghai huo kwani anaye mchumba wake ampendaye kwa dhata huko Undongini. Kitendo cha Maugwaju kuchukuliwa na kupelekwa katika nchi ya kigeni (Bara Arabu), mbali na watu wake, mbali na mchumba wake ndicho kinachomfanya Chonge aone ni fursa pekee ya kumpata Maugwaju kwa hadaa. Msimulizi anasema yafuatayo:

Chonge: Nini mpenzi Amina?

Maugwaju: Sijui Chonge, kifua hiki naona kitaniua.

Chonge: Usiseme hivyo mpenzi. Utapona, usiwe na wasiwasi.

Maugwaju: Chonge, nimechoka kusafiri. Miguu yangu, kifua, mwili wangu wote waniuma.

Chonge: Karibu tutafika Amina. Vumilia (Semzaba, 1984: 18).

Maugwaju: Turudishe Undongini Chonge, mwache Harun. Usiache mbachao kwa msala upitao.

Chonge: (*akiwa imara*) Kurudi haiwezekani.

Matumizi ya nafsi ya kwanza katika kauli za Chonge “... karibu tutafika Amina ...” na Maugwaju “Sijui Chonge... turudishe Undongini...” (Semzaba, 1984: 18) zinadhihirisha ukaribu wa msimulizi katika hadithi ya mapenzi ambayo inasimuliwa. Msimulizi analiunga mkono jambo hili na kutushirikisha uzoefu wake

katika jamii Spines,(2020); Coles (2018); na Mahenge (2019). Vilevile, matumizi ya nasi ya pili kupitia Chonge “usiseme hivyo mpenzi” (Semzaba, 1984: 18) yanatuonesha ukaribu wa msimulizi katika kusimulia hadithi hii kwamba anaunga mkono yanayosimuliwa, na yuko karibu na simulizi kwa maana yuko ndani, na anamtaka msomaji achukue hatua katika kukamilisha simulizi (Matt, 2003; Fludernik, 2006; Mahenge, 2019). Kwa hiyo, mapenzi ni dhamira mojawapo ambayo imetumia nafsi ya kwanza na ya pili kwa malengo mahususi ya msimulizi kama ilivyofafanuliwa hapo juu. Pia, nukuu nyingine inayoonesha dhamira ya mapenzi ni hii hapa:

Maugwaju: ... tazama hali yangu mbovu. Mimi msichana kigori tazama hali yangu ilivyo. Mchafu ninanuka. Sitamaniki. Tazama mzigo wangu. Mkubwa mno uvunjao mgongo wangu kila dakika... (Semzaba, 1984: 17)

Msimulizi anaelezea hisia za ndani za msichana mrembo ambaye kutokana na kutaabishwa na Harun na Chonge, anajikuta katika hali ya uchafu, kunuka na kutotamanika. Kauli zote hizi anazitoa kwa kuegemea nafsi ya kwanza ikionesha msimulizi yuko karibu na simulizi na anaunga mkono yanayosimuliwa.

4.3 Unafiki

Unafiki ni aina nyingine ya dhamira inayojitokeza katika tamthiliya hii. Unafiki unatajwa kama tabia mojawapo ya utumwa kama anavyoelezea Scott (2023) katika andiko lake linalohusu itikadi na unafiki katika mfumo wa utumwa na demokrasia. Unafiki na utumwa vinakwenda pamoja kama anavyoelezea Scott. Hii ni kwa sababu harakati za kupambana na mfumo wa utumwa na biashara ya utumwa, ziligubikwa na unafiki kwa kuwa watu waliokuwa wakipigia kelele mfumo huo ndio wenyewe waliokuwa wakiutekeleza na kuuchochea kutokana na faida zao za kiuchumi. Watu hao walikuwa wakifaidika kupitia biashara ya watumwa na matumizi ya watumwa katika kazi zao za uzalishaji. Unafiki katika tamthiliya hii unajitokeza pale msimulizi kupitia Chonge anapompeleleza Maugwaju kuhusu mipango ya wale watumwa wengine akina Pazi na wenzake baada ya kufahamu kuwa hawaungi mkono suala la Chonge kujipendekeza kwa Harun (Bwana mkubwa) na kumtaka wafanye mapinduzi na watoroke. Chonge anawadodosa watumwa wenzake wa kiume kupitia Maugwaju ambaye anamjibu hivi:

Mugwaju: “Sijui. Wewe dume mwenzao ndio unaweza kujua zaidi yangu. Mie msichana tu, moyo wangu mdogo ...”
(Semzaba, 1984: 18)

Kauli hii inasemwa na msimulizi kupitia Maugwaju baada ya kugundua nia ya Chonge ni kuwasaliti watumwa wenzake badala ya kuungana na kufanya mapinduzi. Msimulizi anatumia nafsi ya kwanza “sijui” ikituonesha kwamba naye

yuko ndani ya simulizi, ni mhusika anayechukua jukumu la kutushirikisha uzoefu wake na anaunga mkono hiyo simulizi. Vilevile, matumizi ya nafsi ya pili “wewe dume mwenzao ndio unaweza kujua zaidi yangu...” yanamaanisha msimulizi yuko karibu na simulizi, anaunga mkono kinachosimuliwa lakini anamtaka msomaji naye achukue jukumu katika kusimulia hadithi hiyo. Matumizi ya nafsi za usimulizi hayatumiki kiholela bali ni kwa makusudi maalumu ya msimulizi. Matumizi hayo yanaweza kutokea katika aina yoyote ya kazi iwe ya kifasihi kama vile riwaya, hadithi, tamthiliya, shairi au filamu (Jann, 2025) au kazi isiyo ya kifasihi kama vile jengo, mashine n.k., lakini inayotoa usimulizi fulani (Bal, 1997). Jengo kama ni nyumba au kibanda, na mashine kama ni ya kusagia nafaka au kukamulia mafuta, huweza kuwa na hadithi ndani yake na msomaji akachambua usimulizi kutokana na jengo hilo au mashine hiyo.

4.3 Utumwa Mkongwe

Utumwa mkongwe ni aina nyingine ya dhamira inayoibuliwa katika uchambuzi huu. Dhamira hii inajitokeza kutokana na Harun kuwakamata watumwa kutoka sehemu mbalimbali za Tanganyika kwa lengo la kuwasafirisha ili waende Bara Arabu, ambako amewaahidia maisha mazuri pamoja na kufumbuliwa macho. Msimulizi kupitia mazungumzo kati ya Chonge na Maugwaju anasema:

Maugwaju: Turudishe Undongini Chonge, mwache Harun. Usiache mbachao kwa msala upitao.

Chonge: (*Akiwa imara*) Kurudi haiwezekani.

Maugwaju: Kwa nini?

Chonge: Nyuma yetu ni giza nene, giza pana.

Maugwaju: Na huko twendako je?

Chonge: Mwanga! Mwangaza! Nuru ya ajabu. Harun amenifumbua jicho moja na jicho langu la pili atalifumbua vilevile!

(Semzaba, 1984: 8)

Msimulizi anatumia nafsi ya kwanza wingi “turudishe Undongini Chonge...” ikimaanishwa kuwa msimulizi anaunga mkono hiyo simulizi. Msimulizi anakubaliana na linalosimuliwa na yeye anajihusisha kwa kutushirikisha uzoefu wake. Kauli hii ya Maugwaju inadhihirisha kwamba watumwa walitolewa katika nchi yao ya Undongini na kupelekwa sehemu tofauti ambayo si kwao. Vilevile, kupitia jibu la Chonge, msimulizi anatumia nafsi ya tatu kuonesha kutokuunga mkono kinachosimuliwa. Matumizi ya nafsi ya tatu katika kauli ya Chonge kwamba “Harun amenifumbua jicho moja na jicho langu la pili atalifumbua vilevile”, inatodokezea jambo muhimu katika Nadharia ya Naratolojia kwamba msimulizi yuko nje ya simulizi. Msimulizi amejiweka pembeni kama mtazamaji na siyo mhusika katika kusimulia hadithi hiyo. Hii inamaanisha kwamba msimulizi ‘hakubaliani’ na hilo wazo, na hivyo, anachukua hatua ya kujitoka na kwa kutumia

nafsi ya tatu anatuonesha kwamba hakubaliani na tukio hilo la kitumwa la kupeleka watu uhamishoni.

4.5 Ukombozi wa Fikra

Dhamira nyingine ni ukombozi wa kifikra ambao unaweza kutazamwa kupitia mazungumzo ya Pazi na wenzake wanapojitafakari hali yao na kuona wanatakiwa kuchukua hatua. Mtu pekee wa kufanikisha mpango wao ni Maugwaju ambaye bado ana ari ya kurudi kwao Undongini. Ila hofu inawaingia baada ya kuujua ukweli kwamba Chonge amekuwa akimsemeshasemesha Maugwaju, na huenda amefanikiwa kuugeza moyo wake, hivyo, huenda Maugwaju asiwe upande wa akina Pazi wa kukataa kusahaulishwa asili yao pamoja na kukataa kupelekwa utumwani. Msimulizi anasema:

- Ngati: Tutasahauje asili yetu?
 Pazi: Kwa kuwa na majina na dini na mambo mengine tusiyoyafahamu
 Ngati: Hata hivyo wataweza kubadili kila kitu chetu lakini hawataweza kubadilisha weusi wa ngozi zetu
 Pazi: Umesema kijana. Katu hawataweza kubadili rangi yetu na hivyo hawataweza kutufanya kusahau asili yetu
 Tendegu: Lakini mbona yule pale anaonekana kusahau asili yake? Mwone anajitenga nasi na kazi yake ni kutuangamiza sisi na asili yake (Semzaba, 1984: 17)

Mazungumzo haya kati ya Pazi, Tendegu na Ngati ambayo yanatumia nafsi mchanganyiko zinazotupatia tafsiri mbalimbali. Mosi, kuna matumizi ya nafsi ya kwanza wingi kupitia kauli ya Ngati “tutasahauje asili yetu” (Semzaba, 1984: 17). Hii inatufanya tumwone msimulizi kuwa yuko ndani ya simulizi. Msimulizi anachukua nafasi katika kusimulia hadithi hii ya ukombozi wa kifikra na kwa mujibu wa Nadharia ya Naratolojia, msimulizi akiitumia nafsi ya kwanza katika kusimulia, inamaanisha kwamba msimulizi yuko ndani ya simulizi, anaunga mkono yanayosemwa na anakubaliana nayo kwa kuwa anatupatia uzoefu wake (Spines, 2022; Coles, 2018; Mahenge, 2019). Vilevile, msimulizi anatumia nafsi ya pili kupitia Pazi “umesema kijana...” akiunga mkono wazo alilolitoa Ngati kwamba hata wakitafuta namna ya kusahaulisha mtu na asili yake au kumbadilisha jina, kamwe hawawezi kubadilisha rangi ya ngozi yake. Matumizi ya nafsi ya pili yanamaanisha kwamba msimulizi yuko ndani ya simulizi, anaunga mkono yanayosimuliwa na anamtaka msomaji achukue jukumu la kusimulia hadithi hiyo (Matt, 2003; Fludernik, 2006; Mahenge, 2019). Hata vivyo, katika mazungumzo hayo kunajitokeza nafsi ya tatu kupitia Tendegu anayesema, “Lakini mbona yule pale anaonekana kusahau asili yake? Mwone anajitenga nasi...”. Kwa kutumia nafsi ya tatu ya usimulizi, maana yake msimulizi yuko nje ya simulizi, amejitenga na haungi

mkono jambo linalosimuliwa. Hapa tunaona jinsi msimulizi asivyokubaliana na masuala haya ya kutokujitambua pamoja na utumwa.

4.6 Mapinduzi

Mapinduzi ni aina nyingine ya dhamira inayojitokeza katika uchambuzi wetu. Wahusika Pazi, Tendegu na Ngati, wanajitoa mhanga kwa kutaka kufanya mapinduzi ili wajikombole bila kuogopa au kujali kitisho chochote. Watumwawaa wanasuka mpango wa kumuua Harun ila wanakosoana na kutaka kuwa na tahadhari kidogo kwa kuwa mwanzoni mpango huo ulimjumuisha Chonge na Maugwaju. Hata hivyo, kutokana na unafiki na usaliti, Chonge anajiona bora na kuungana na Harun, hivyo, kuwa kinyume na watumwa wenzake. Hivyo, mazungumzo yanapangwa na mtu wa kufanikisha mpango wa kumuua Chonge ni Maugwaju kama inavyoonekana hapa chini:

- Pazi: Mtu wetu ni Maugwaju, na bado ana ari ya kurudi. Tumtumie.
- Tendegu: Tutamtumiaje na hali wakati wote yeye na Mabruki wako kama chanda na pete? Pia tutajuaje mambo yao? Pengine Maugwaju amebadili nia yake baada ya kushawishiwa na Chonge. (Semzaba, 1984: 18)

Watumwa hawa wanawasiliana na Maugwaju na mpango unasukwa. Ili kutekeleza mpango huo, Maugwaju anatafuta namna ya kuwa na 'uhuru' kwa kutuliwa mzigo ili aweze kufanya jambo la kishujaa analolifikiria. Pamoja na kutuliwa mzigo, Maugwaju anataka kamba ya shingoni ifunguliwe ili aweze kutembea vizuri naye 'aone nuru' kama Chonge. Mwandishi anatupatia maelezo ya jukwaani kabla msimulizi hajasimulia hadithi hii kupitia mazungumzo ya Chonge na Maugwaju. Mwandishi anasema: *watumwa wanaamka. Wanajitayarisha kuanza safari. Maugwaju hana chochote. Yuko mbele ya msafara. Anakohoa kwa nguvu. Chonge anamfuata*)

- Chonge: Nini mpenzi Amina?
- Maugwaju: Sijui Chonge, kifua hiki naona kitaniua.
- Chonge: Usiseme hivyo mpenzi. Utapona, usiwe na wasiwasi.
- Maugwaju: Chonge, nimechoka kusafiri. Miguu yangu, kifua, mwili wangu wote waniuma.
- Chonge: Karibu tutafika Amina. Vumilia.
- Maugwaju: Turudishe Undongini Chonge, mwache Harun. Usiache mbachao kwa msala upitao.
- Chonge: (*akiwa imara*) Kurudi haiwezekani

(Semzaba, 1984: 18)

Matumizi ya nafsi ya pili kupitia kauli ya Chonge: "Usiseme hivyo mpenzi. Utapona, usiwe na wasiwasi", yanatupeleka kwenye tafsiri ya Fludernik (2006)

kwamba msomaji anahusishwa ili achukue majukumu katika kusimulia hadithi. Fludernik (2006) anaendelea kueleza kuwa msimulizi akitumia sana nafsi ya pili pamoja na njeo ya wakati uliopita, ndipo msomaji halisi (kwa maana yule ambaye amekishika kitabu na anakisoma) anapogutuka na kufahamu kuwa msimulizi hazungumzi na yeye bali anazungumza na msomaji wa kufikirika ambaye (mwandishi na msimulizi) walimfikiria walipokuwa wanaiandika na kuisimulia kazi yao. Lakini endapo msimulizi anatumia wakati uliopo, inamfanya msomaji ajione anasemeshwa yeye (Fludernik, 2006; Mahenge, 2019). Baada ya majibizano hayo, Amina (Maugwaju) anamwomba Chonge afunguliwe kamba ya shingoni ili kudhihirisha kama kweli anampenda kwa dhati. Kutokana na ‘mtego’ huo wa maneno ya Amina (Maugwaju), Chonge anamfungulia ile kamba ya shingoni na Amina anakuwa huru huku akiuongoza msafara wa watumwa wenzake akiwa hajabeba mzigo wowote na hajafungwa kamba shingoni. Maugwaju anarudia kuwafundisha wenzake wimbo wa ukombozi bila ya kujali ukatili huo wa kibinadamu ambao Pazi na wenzake waliupata kwa kuimba wimbo huo. Maugwaju anaambisha wimbo kama ifuatavyo:

*Ingawa nimetengwa nawe
Nikufikiriapo furaha hainiishi moyoni.
Sijui kama tutaonana tena
Ee Undongi nchi yangu
Undongi ya amani na furaha
Mihogo yako mitamu
Undongi nchi yangu ya asali isiyo na mfanowe
(Semzaba, 1984: 8)*

Baada ya Maugwaju kuwafundisha wimbo huo wanaweza kuuimba vizuri na kwa nguvu. Chonge anahamaki anapobaini kwamba mwimbishaji ni mpenziwe Amina, kwani ametoka kuwakanyaga wanaume wenzake mpaka wamezimia kwa kosa la kuimba wimbo wa “Undongini” badala ya wimbo wa “Tende na Harua”. Chonge anawafuata watumwa kwa haraka lakini kabla hajachukua hatua yoyote ya kumkabili ‘mpenzi wake’, Amina/Maugwaju anamfyatulia risasi Chonge na kumuua. Naye Harun anapokuja kushangaa, anafyatuliwa risasi na wote wanakufa hapohapo. Hatimaye watumwa wakawa huru, wakarudi kwao Undongini.

Kama ilivyoelezwa katika sehemu iliyotangulia hapo juu, wimbo wa ukombozi pamoja na mazungumzo yaliyozalisha ukombozi huo, yanawasilishwa kwa kutumia mbinu ya usimulizi ya nafsi ya kwanza (umoja au wingi) ikituthibitishia kwamba msimulizi ni sehemu ya simulizi, yuko ndani ya simulizi akitimiza majukumu kama mhusika (Spines, 2022; Coles, 2018; Mahenge, 2019). Msimulizi anakubaliana na yanayosimuliwa na yeye ni mhusika katika kutekeleza majukumu hayo. Hii inatupa tafsiri kwamba msimulizi anaunga mkono harakati za mapinduzi na harakati za ukombozi ili watumwa waachiwe huru.

5.0 Mjadala na Matokeo ya Utafiti

Matokeo ya uchambuzi wa makala haya yanaonesha jinsi dhamira mbalimbali zinavyoweza kuibuliwa kupitia matumizi ‘mahususi’ ya sauti za usimulizi. Kupitia mbinu hizi za usimulizi, tumeweza kufahamu kama msimulizi anaunga mkono yanayosimuliwa, anamshirikisha msomaji na msikilizaji, au anayapinga yanayosimuliwa. Mjadala huu tumeugawa katika hoja tatu ambazo zinatokana na matumizi ya sauti za usimulizi kwamba msimulizi anaunga mkono, haungi mkono, au anajitenga na simulizi.

Msimulizi anaunga mkono yanayosimuliwa kupitia dhamira ya mapenzi, ukombozi wa fikra na mapinduzi ambazo zinawasilishwa kwa kutumia nafsi ya kwanza. Msimulizi kupitia Maugwaju anasema kwamba: “ninanuka...sitamaniki” ikimaanisha kwamba (yeye) msimulizi ni sehemu ya simulizi hii (Spines, 2022; Coles, 2018; Mahenge, 2019). Pia, kupitia dhamira ya ukombozi msimulizi anatusimulia kwa kusema “mtu wetu ni Maugwaju...tumentie”. Msimulizi katika miktadha yote hii miwili ni mhusika ambaye yuko ndani ya simulizi na anatushirikisha uzoefu wake katika mapenzi na ukombozi dhidi ya utumwa. Hivyo, matumizi hayo yanaonesha yuko “hai” katika kusimulia hadithi (Mahenge, 2019). Kwa kuwa hai na kutumia nafsi ya kwanza [umoja au wingi] inatueleza kuhusu msimulizi kuunga mkono yale yanayosimuliwa hadithini.

Msimulizi anatumia nafsi hii katika udodosaji wa habari za watumwa ili amshirikishe msomaji katika kuwachongea watumwa wenziwe kwa Haruni. Hoja ya kumshirikisha msomaji na msikilizaji ili wachukue hatua fulani katika kukamilisha simulizi inajitokeza kupitia matumizi ya nafsi ya pili ya usimulizi. Katika tamthiliya hii ya *Tendehogo*, tunaona Maugwaju akimsemesha Chonge kwamba: “wewe dume mwenzao ndiyo unaweza kujua zaidi yangu” ikimaanisha kuwa msimulizi anaongea na hadhira ya wasomaji na wasikilizaji na kuishirikisha katika kusimulia hadithi hiyo, kwamba wachukue hatua fulani. Matumizi ya nafsi ya pili yanamaanisha msimulizi yuko karibu, hivyo, yuko “hai” katika kusimulia na anamshirikisha msomaji ili washirikiane kusimulia (Matt, 2003; Wiehardt, 2018; Mahenge, 2019).

Msimulizi haungi mkono yanayosimuliwa kuhusiana na kushabikia utumwa mkongwe na usaliti. Hoja hii ya kutokuungwa mkono kwa yale yanayosimuliwa katika simulizi, yanajidhihirisha kupitia kauli ya Chonge juu ya msimamo wa watumwa kutoroka ambapo anasema: “Achana na mipango isiyo na misimamo watamuweza wapi Harun”. Hii inamaanisha kuwa, msimulizi yuko nje ya simulizi, anaitazama kama mtazamaji (Prudchenko, 2017; Mahenge, 2019). Msimulizi amejitenga na kwa hiyo yanayozungumziwa hakubaliani nayo na hayaungi mkono. Kwa maana nyingine, msimulizi hayuko hai, yaani katika kusimulia (Boyd, 2018; Bonn, 2018). Jambo hili linamaanisha amejitenga na mambo yanayosemwa na, kwa hiyo, hayaungi mkono (Mahenge, 2019). Hii ni kwa kuwa yeye amekaa pembeni anajiondoa kuwa sehemu ya usaliti na unafiki kama unavyodhihirika kupitia Chonge asiyejitambua.

6.0 Hitimisho

Makala hii imetumia msingi mmoja wa Nadharia ya Naratolojia ambao ni usimulizi kubainisha msimulizi, namna anavyosimulia, anachosimulia na maana inayoibuliwa kupitia matumizi hayo. Ili kufikia katika lengo hilo, tulichunguza nafsi za usimulizi, yaani nafsi ya kwanza, ya pili, na ya tatu zinavyojitokeza katika tamthiliya ya *Tendehogo*. Matumizi ya nafsi hizi yana maana yake mahususi inayoibuliwa kwa kuwa hubainisha ni “nani” anayesema na “kwa nini” anasema hayo ayasemayo na vilevile “anayasemaje”. Matumizi ya nafsi ya kwanza katika usimulizi humaanisha kwamba msimulizi yuko ndani ya simulizi, anaunga mkono yanayosemwa na anakubaliana nayo (Spines, 2022; Coles, 2018; Mahenge, 2019). Uchambuzi umebaini kwamba mambo ambayo msimulizi anayaunga mkono na kuyakubali ni mapenzi, mapinduzi na ukombozi dhidi ya utumwa.

Matumizi ya nafsi ya pili yanamaanisha msimulizi anamshirikisha msomaji ili naye atimize majukumu mbalimbali (Matt, 2003; Wiehardt, 2018; Mahenge, 2019). Pia, ni njia inayotumika kumaanisha mazungumzo au mawasiliano kati ya pande mbili, anakuwapo mzungumzaji na pia anakuwapo msikilizaji. Katika uchambuzi wetu tumekutana na kauli ambazo msimulizi anatumia nafsi ya pili na hii ni kwa yale mambo ambayo anataka kumshirikisha msomaji au msikilizaji ili achukue hatua katika kusimulia hadithi. Matumizi haya yametumika katika sehemu ambazo kuna udodosaji wa taarifa za watumwa.

Matumizi ya nafsi ya tatu yanamaanisha msimulizi amejitenga na simulizi na hayaungi mkono yanayosemwa (Prudchenko, 2017; Mahenge, 2019). Katika uchambuzi wetu tumeona kwamba usaliti, unafiki na kutojitambua ni baadhi ya mambo ambayo msimulizi hayaungi mkono na hakubaliani nayo kwa jinsi yanavyotendeka, hivyo, ameyasimulia kwa kutumia nafsi ya tatu.

Matumizi haya ya sauti za usimulizi siyo ya bahati mbaya bali msimulizi anapoyatumia kuna maana inayoibuliwa ikiwa ni ama kuyaunga mkono au kutaka ushirikishaji au kuyapinga. Sauti za usimulizi zinaweza kuchunguzwa katika kazi yoyote ile iwe ya kifasihi au isiyo ya kifasihi. Jambo kubwa linalotazamwa ni kuwapo kwa simulizi. Matumizi haya ya nafsi za usimulizi yamesaidia kuibusha dhamira mbalimbali kama ilivyoelezwa hapo juu.

Mapendekezo yanayotolewa na utafiti huu ni kufanya utafiti mwingine katika tamthiliya ya *Tendehogo* ili kuchunguza namna sauti za usimulizi zinavyoweza kuibua aina mbalimbali za utumwa.. Inapendekezwa itumike Nadharia ya Naratolojia ili kuona kama usimulizi unaweza kusaidia kubaini aina nyinginezo za utumwa hususani kubaini kama msimulizi anajipatanisha na simulizi, anamshirikisha msomaji ili achukue hatua, au amejitenga na kuwa mtazamaji akiangalia yale yanayotokea bila kuyaunga mkono.

Marejeleo

- Altman, R. (2008). *A Theory of Narrative Structure*. New York: Columbia University Press.
- Bal, M. (1997). *Narratology Introduction to the Theory of Narrative*. 2nd edition. Toronto: University of Toronto Press.
- BAKITA (2015). *Kamusi Kuu ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Longhorn Publishers.
- Bonn, A. (2018, h.t). "Role of Narrator in American Novel". Retrieved from <https://study.com/academy/lesson/role-of-the-narrator-in-american-novels-types-and-examples.html>.
- Boyd, B. (2018, September 5). "Role of the Narrator in British Novel Types & Examples". Retrieved from <https://study.com/academy/lesson/role-of-the-narrator-in-british-novels-types-examples.html>.
- Bordwell, D. (1985). *Narration in the Fiction Film*. Madison: University of Wisconsin Press.
- Coles, W.H. (2018, h.t). 1stPerson POV in Literary Story. Retrieved from <https://www.storyinliteraryfiction.com/essays-on-writing/1st-person-pov-in-literary-story>
- Fludernik, M. (2006). *An Introduction to Narratology*. London: Routledge.
- Genette, G. (1980). *Narrative Discourse: An Essay on Method* (Kimetafsiriwa na Jane E. Lewin). Ithaca: Cornell University Press.
- Henry, G. (2020). Uchambuzi Linganishi wa Ujumi wa Kifasihi katika Simulizi Teule za Watumwa Kutoka Afrika, Amerika na Ulaya. Tasinifu ya ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Herman, L. na Vervaeck, B. (2005). *Handbook of Narrative Analysis*. Lincoln: University of Nebraska Press.
- Hubert, H.W. (2016). Assessing the Role of the Narrator in the Verse Novel: A Look at Pushkni's Eugene Onegin. Tasinifu ya Umahiri (haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Ghana.
- Jann, M. (2005, May 8). Narratology: A Guide to the Theory of Narrative. English Department, University of Cologne. Retrieved from [Jahn, Manfred - Narratology-A Guide To The Theory of Narrative PDF | PDF | Narration | Narrative](#)
- Jahn, M. (2025). Narratology 3.0: A Guide to the Theory of Narrative. English Department, University of Cologne. Retrieved from www.uni-koeln.de/~ame02/pppn.pdf.
- Madumulla, J.S. (2009). *Riwaya ya Kiswahili Nadharia, Historia na Misingi ya Uchambuzi*. Dar es Salaam: Mture Educational Publishers Limited.
- Madumulla, J.S. (2000). *Riwaya ya Kiswahili: Nadharia, Historia na Misingi ya Uchambuzi*. Nairobi: Phoenix Publishers.
- Mahenge, E.G. (2019). Uumbaji wa Ualbino Katika Fasihi ya Kiswahili: Uchambuzi wa Kazi Teule. Tasinifu ya Uzamivu (haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

- Matt, D. (2003). "The influence of Narrative Tense in Second Person Narration: A Response to Joshua Parker". *Connotations*. 23(1): 55-62.
- Miers, S. (2000). "Contemporary Forms of Slavery". *Canadian Journal of African Studies*. 34 (3): 714-747.
- Mlacha, S.A.K. (1991). "Point of View as Stylistic Device in Kiswahili Novels". *Jarida la TUKI la Kiswahili*. (58): 54-61.
- Mohochi, E.S. (2000). "Usimulizi wa Riwaya ya Nyongo Mkalia Ini". *Nordic Journal of African Studies*. 9(2): 49-59.
- Mulokozi, M.M. (2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: KAUTTU.
- Mulokozi, M.M. (2020). "Makala Elekezi: Kiswahili na Umajumui wa Kiafrika". https://www.google.com/search?q=umajumui+wa+kiafrika+mulokozi+chaukidu&rlz=1C1WNOO_enZA1137ZA1137&oq=umajumui+wa+kiafrika+mulokozi+chaukidu&gs_lcrp=EgZjaHJvbWUyBggAEEUYOTIHCAEQIRigATIHCAlQIRigAdIBCjE1OTI5ajBqMTWoAgiwAgHxBVi3aqwZ3DPA&sourceid=chrome&ie=UTF-8#vhid=zephyr:0&vssid=atritem-https://journals.udsm.ac.tz/index.php/mj/article/view/1712/1591
- Mutembei, A. (2016). "Slavery and Its Space in Kiswahili Literature". *Asian Journal of African Studies*. 39: 1-32. Retrieved from <https://www.kci.go.kr/kciportal/ci/sereArticleSearch/ciSereArtiView.kci?seReArticleSearchBean.artiId=ART002107043>.
- Prudchenko, K. (2017). "Pen and the Pad: The Difference between an Observer and a Participant in a Narrative". Retrieved from <http://penandthepad.com>.
- Semzaba, E. (1984). *Tendehogo*, Dar es Salaam: Tanzania Publishing House.
- Semzaba, E. (1977). *Tamthiliya ya Kiswahili*, Dar es Salaam: Open University of Tanzania.
- Scott, S.J. (2023). "Ideology and Hypocrisy Amid Slavery and Democracy Strange Bedfellows from Time Immemorial". Retrieved from <https://www.hamptonthink.org/read/ideology-and-hypocrisy-amid-slavery-and-democracy-strange-bedfellows-from-time-immemorial>
- Spines, (2022, June 6). First Person Narrative: Definition, Examples, and Writing Tips for a Strong Perspective. Retrieved from <https://spines.com/writing-a-first-person-narrative>
- TUKI (2019). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: Oxford University Press.
- Van der Linden, M. (2016). "Dissecting Coerced Labor." Katika M.M. van der Linden na M.R. García (Wah.), *On Coerced Labor: Work and Compulsion after Chattel Slavery*. 293–322. Leiden: BRILL. Retrieved from <https://doi.org/10.1163/9789004316386>.
- Welch, C.E. (2019). "Defining Contemporary Forms of Slavery: Updating a Venerable NGO". *Human Rights Quarterly*. 31(1): 70-128

Wiehardt, G. (2020, July 17). Second – Person Point of View. Retrieved from <https://www.liveabout.com/the-second-person-point-of-view-in-fiction-writing-1277131#>